# LENGO LA MAKAMBI NA JINSI YA KUENDESHA







# Makabrasha Ya Roho Ya Unabii Kuhusu Mkutano Wa Makambi

(CampMeetings)

Kimetafsiriwa kutoka *Camp-Meetings: Their Object, and How to Conduct Them*

*Kitini Hiki Bado Ni Rasimu (Jaribio La 1)*

Ellen G. White

1900

Copyright © 2018
Ellen G. White Estate, Inc.

YALIYOMO

**Wafanikishaji Wa Kazi (Watafsiri, Wahariri, Waombezi, Washauri, Wasanifu n.k.)**........................................................2

**Maneno Ya Wafanikishaji wa Kazi**............3

**Kufikia Watu Wengi**................................14

**Kielelezo**..............................................17

**Jinsi ya Kuhakikisha Mahudhurio**............19

**Washiriki wa Makanisa Yetu Wanapaswa Kuhudhuria Mkutano wa Makambi**.........25

**Maandalizi Ya Moyo Yahitajika**..............30

**Biashara Ziahirishwe**...............................36

**Msaada wa Wachungaji**...........................40

**Wote Wawe Watendakazi**........................45

**Sala na Ushauri wa Mara kwa Mara**........47

**Haja ya Kanisa**.........................................52

**Jinsi Ya Kuwasilisha Ukweli**...................54

# Wafanikishaji Wa Kazi (Watafsiri, Wahariri, Waombezi, Washauri, Wasanifu n.k.)

Grace Momadi Masaka-New Jersey, Marekani,

Daniel Nyangaresi Masaka - Kisii, Kenya,

Gerard Odot Nyafanga - Rorya, Tanzania

Musa L. Budodi-Shinyanga, Tanzania

Faustine Momadi Mkama - Dar, Tanzania

Mbusi Mpagalushu - Bariadi, Tanzania

David Jabez Masaka - Pennsylvania, Marekani

Paul Momadi Masaka - New Jersey, Marekani

Obadiah Murimi -Nakuru, Kenya

Esrom Katuma - Mara, Tanzania

Judi na John Mugane – Boston, Marekani

Robert Ndinayo - Congo DRC

Wilson Gibson Mujuni - Kagera, Tanzania

Paul Nsulwa - Mafinga, Tanzania

Samaritan Laymen Ministries, New Jersey

Isack Msusu-Kigoma, Tanzania

Luwela Elias-Rukwa, Tanzania

Vitabu Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

RYU na Runinga ya Upendo

# Maneno Ya Wafanikishaji wa Kazi

Tumetafsiri kama Wikipedia, yaani mtu anayefuata anaboresha zaidi. Na tualike watu kuja kambi msimu huu!

Siku kuu ya mahema (vibanda/makambi) ilikuwa ni kivuli tu ambapo kitu halisi ni pale katika ujio wa Yesu mara ya pili na kukambika kwa watakatifu miaka 1000 (Milenia) mbinguni kisha kurudi kwenye makao ya milele duniani katika nchi mpya.

Mwaka wa kiyahudi, kidini ulikuwa na miezi 7 tu, ukianza mwishoni mwa mwezi wa 3 na mwanzoni mwa mwezi wa 4 kwa kalenda ya sasa, na ukiishia mwishoni mwa mwezi wa 9 na mwanzoni mwa mwezi wa 10 kwa kalenda ya sasa. Sikukuu zote zilipaswa kuadhimishwa ndani ya miezi 7, kuanzia mwezi Abibu hadi mwezi Tishri, lakini ilikuwepo miezi 12 kwa mwaka.

- **Pasaka** (ishara ya Kifo cha Yesu)
- Mikate Isiyotiwa Chachu (Ishara ya Mazishi ya Yesu)
- Malimbuko (Ishara ya Kufufuka kwa Yesu)

- Pentekoste (Yesu kuhani akihudumu katika chumba cha kwanza cha patakatifu)
- Mabaragumu (Ishara ya Tangazo la mwanzo wa hukumu ya mwisho mbinguni)
- **Siku Kuu ya Upatanisho** (Ishara ya Hukumu kuu mbinguni)
- **Vibanda/Makambi** (Ishara ya Miaka 1000 mbinguni—Milenia)

Kama ilivyokuwa zamani (Walawi 23:40-43), leo watu wa Mungu, baada ya mavuno, twakaa nje ya majumba yetu na kwenda kwenye makao ya mahema kwa siku 7. Mavuno ni mfano (type) wa mavuno ya watu watakaofaa katika marejeo ya pili (antitype), na wakusanyaji si wengine zaidi ya malaika; baada ya mavuno hayo, hatimaye kambi la mbingu kwa muda wa miaka 1000.

> *"Sikukuu hii ilikuwa hususani fursa ya kufurahi. Ilifanyika baada tu ya siku ile kuu ya upatanisho, pale hakikisho lilikuwa limetolewa kwamba uovu wao usikumbukwe tena. Wakiwa wamepatana na Mungu, sasa walimjia mbele Zake kushukuru wema Wake na kumsifu kwa ajili ya rehema Yake." Wazee na Manabii, sura ya 52, uk. 540 Aya ya 18.*

*"Vile ilivyokuwa pasaka, siku kuu ya vibanda ilikuwa yenye kukumbukwa. Katika kukumbuka kusafiri kwao nyikani sasa watu walipaswa kuyaacha makao yao na kwenda kukaa katika vibanda au mahema, vilivyotengenezwa kwa matawi ya 'miti mizuri, na matawi ya mitende,na makuti. Walawi 23:40, 42, 43. Ibid Aya ya 19.*

**Millennium** ni neno lililotoholewa toka katika maneno mawili ya Kilatini, "**Mille**"-likimaanisha **Elfu** na "**Annum**" likimaanisha **Mwaka**. Neno hili halipatikani katika Biblia bali limekuja kuwa na maana fulani katika akili za Wakristo wengi kama kipindi cha miaka 1000 ambapo Kristo atatawala pamoja na watakatifu wake. Utawala wa miaka elfu wa watakatifu pamoja na Kristo umenenwa katika Kitabu cha Ufunuo 20:2-7 ambapo watatawala wakiwa mbinguni.

**Uhusiano Wa Kipindi Cha Milenia** (Kikwi) **Na Matukio Mengine Ya Mwisho Wa Historia Ya Ulimwengu** (Eschatological Events).

Ufunuo 19 huonyesha marejeo ya pili ya Bwana wetu. Sura ya 20 huongelea:

1. Ufufuo wa kwanza

2. **Kufungwa kwa Shetani hapa duniani kwa miaka elfu (huku mbinguni watakatifu wakitawala pamoja na Kristo)**
3. Ufufuo wa pili usio heri, hukumu jumuishi ya watenda maovu, na kuangamizwa kwao katika ziwa la moto.

Ufunuo 21 hutoa picha ya namna mji mtakatifu utakavyoshuka, Yerusalemu mpya; na Ufunuo 22 huendelea kuufafanua mji na shangwe ya waliokombolewa wakiwa katika hali ya umilele (immortality).

## Mtiririko Wa Matukio Yanayohusiana Na Kipindi Cha Milenia.

### 1. Marejeo Ya Pili Ya Kristo.

Katika Ufunuo 19 Kristo anaonyeshwa katika marejeo yake ya pili **kama shujaa mwenye uweza akiongoza majeshi ya mbinguni kupigana dhidi ya majeshi ya waovu** (fungu la 11-16). Hii hutoa mkazo juu ya matokeo ya ujio Wake juu ya wasiokuwa wameokolewa.

Katika **Ufunuo 14 Kristo anaonyeshwa akija juu ya wingu, amevikwa taji ya dhahabu kama Mfalme wa wafalme**. Katika Sura hii kukusanywa kwa wenye haki na waovu **unaonyeshwa katika lugha ya picha**, yaani "**mavuno**". Katika fungu la 15 na 16 wenye haki wanakusanywa kama "**mavuno ya nchi**." Pia (katika mafungu 18 na 19) waovu wanavunwa kama "**vichala vya mzabibu wa nchi**"-"**zikiwa zimeiva sana**." Na Kristo anaamuru "**zitupwe katika shinikizo lile kubwa la ghadhabu ya Mungu**." Shinikizo hili limetajwa pia katika Sura ya 19, ambapo Kristo "**anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi**" (Fungu la 15).

Wakati wa mavuno ni wakati ambapo kipimo cha dhambi za wanadamu zimefikia ujazo wake, na wadhambi wameiva tayari kwa kuangamizwa; maadui wa Kristo hawaangamizwi mpaka pale dhambi zao zimeiva kwa ajili ya kuangamizwa, naye ataivuna nchi ipumzike kwa milenia (kikwi) moja sawa na vile Mungu alivyowaagiza wana wa Israeli kuwa wangeilima ardhi kwa miaka 6 na wa

7 waiache ipumuzike, ndivyo pambano kati ya giza na nuru katika dunia yetu lipo kwa miaka 6000 na miaka 1000 ni ya dunia hii kuachwa ipumzike kukamilisha namba 7 kama ilivyo kanuni ya Mungu tangu zamani, yaani 6 kwa wanadamu na ya 7 ni kwa Muumbaji.

*Nini Maana Ya Shinikizo?*

*a. Ni tendo la kulazimisha jambo lifanyike,*

*b. Ni malumbano ya nguvu ya kumbana mtu, shirika au serikali itekeleze jambo fulani,*

*c. Ni hali ya kubinya kwa nguvu,*

*d. Katika nyakati za zamani, shinikizo lilikuwa ni* ***shimo*** *lililochimbwa (angalia Isaya 5:2), kimo futi 2 au 3 ambapo chini yake kuna mwamba, yalikuwa yakichimbwa mashimo mawili (yakiunganishwa na bomba) kwa ajili ya kubinya au kukamua zabibu itoe sharubati/divai mpya (angalia Isaya 63:1-3). Divai ilitiririka kutoka shimo moja kwenda jingine kupitia bomba na kisha kuhifadhiwa kwenye chungu au popote ilipopaswa kutunzwa.*

Lakini kama neno hili lilivyotumika katika makala

hii hapo juu, neno **shinikizo** maana yake ni shimo au mahali ambapo baada ya miaka elfu moja (milenia) waovu wote wataangamizwa, ni shimo ambamo ghadhabu ya hasira ya Mungu itamwagwa.

## 2. Kufa Kwa Wadhambi Wote.

Kwa wadhambi wote Kristo anakuja kama mhukumu, katika utukufu mkuu mno hata asili inakuwa na ghasia baada ya kuonekana kwa Kristo mawinguni katika marejeo ya pili, mbingu zinakunjamana kama ukurasa, milima na visiwa vinahama kutoka sehemu zake (Ufunuo 6:14-17).

Katika Sura ya 14 na 19 ya kitabu cha Ufunuo, matokeo ya ujio wa Kristo juu ya waovu unafafanuliwa katika lugha ya picha, yaani kuzikanyaga zabibu katika shinikizo, huku damu zao zikitoka nje ya shinikizo (shimo) zikisambaa nje ya shinikizo (Ufu. 14:20).

Mnyama pamoja na nabii wa uongo (ishara ya muungano wa uasi) wanatuhumiwa kwa

kuwadanganya waovu katika kudumu kuasi dhidi ya Mungu, na wanaonyeshwa wanatupwa katika ziwa la moto (Ufunuo 19:20) baada ya miaka 1000. Paulo mtume, akitazama mbele kwa jicho la kinabii alifafanua Siri ya kuasi "ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa Chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo Kwake."

(2 Thes. 2:8) Na Ufunuo 19 inamalizia ufafanuzi wa maangamizi jumuishi ya waovu kwa maneno haya, "na wale waliosalia [wadhambi waliosalia] waliuawa kwa upanga Wake Yeye aliyeketi juu ya yule farasi, upanga utokao katika kinywa Chake. Na ndege wote wakashiba kwa nyama zao." (fungu la 21)

## 3. Kufungwa Kwa Shetani

Tukio la mwisho linalofafanuliwa katika Ufunuo 20:1-3 ni kufungwa kwa shetani kwa mnyororo. Kwa sababu hili ni tukio la mfano/ishara (symbolic scene), haina maana ya kuwa mnyororo au shimo la kuzimu ni vitu halisi, kwani hata shetani mwenyewe kawakilishwa kama joka. Katika wakati huu wafuasi wote wa shetani wameangamizwa katika ujio wa pili wa

Kristo na wenye haki wameondolewa kwake, dunia imekuwa ukiwa mkuu.

Mikutano yetu ya makambi ni mojawapo ya mawakala muhimu katika kazi yetu. Ni mojawapo ya mbinu bora zaidi za kuvuta usikivu wa watu, na kufikia matabaka yote kwa mwaliko wa injili. Wakati tunaoishi ni wakati wa amsha-amsha kuu. Tamaa, vita, anasa na kutafuta pesa, huteka akili za watu. Shetani aona kwamba wakati wake u mfupi, na ameweka mawakala wake wote kufanya kazi ili watu wapate kudanganywa, kulaghaiwa, kutingwa, na kupokonywa akili zao mpaka kipindi cha rehema kwisha na mlango wa rehema kufungwa milele. Ni kazi yetu kuupa ulimwengu wote—kwa kila taifa, kabila, lugha, na jamaa—zile kweli ziokoazo za Ujumbe wa Malaika yule wa Tatu. Lakini imekuwa ni tatizo gumu kujua jinsi ya kuwafikia watu katika vituo vyenye watu wengi. Hatupatiwi kibali cha kuingia makanisani. Katika miji mikubwa kumbi za mikutano ni ghali, na katika hizo kumbi bora ni wachache tu kwa kawaida huja kusikiliza ujumbe. Tumesemwa vibaya na

wale ambao hawakutufahamu. Sababu za imani yetu hazieleweki kwa watu, na tumechukuliwa kama washupavu, na ambao kwa ujinga walikuwa wakitunza Jumamosi badala ya Jumapili. Katika kazi yetu tumefadhaishwa katika kujua jinsi ya kuvunja vizuizi vya ulimwengu na ubaguzi na kuleta mbele ya watu Ukweli wa thamani ambao una maana kubwa sana kwao. Bwana ametuagiza kwamba mikutano ya kambi ni mojawapo ya nyenzo muhimu zaidi za kukamilisha kazi hii. (*Msisitizo: Je, unaalika rafiki zako wasio wakristo kwenye mkutano wa kambi*). PH130 1.1

Ni lazima tubuni, na kupanga kwa busara, ili watu wapate fursa ya kusikia wenyewe ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Watu wanapaswa kuonywa ili wajitayarishe kwa ajili ya siku kuu ya Mungu ya hukumu, iliyo juu yao. Hatuna muda wa kupoteza. Ni lazima tufanye kila tuwezalo kuwafikia watu pale walipo. Ulimwengu sasa unafikia ukomo, ukiwa na moyo mgumu na kutokujali sheria za serikali ya Mungu. Katika kila mji wa

ulimwengu wetu onyo lazima litangazwe. Yote yanayoweza kufanywa yafanyike bila kuchelewa. PH130 2.1

Na mikutano yetu ya kambi ina kusudi jingine, yaani maandalizi kwa ajili ya hili. Inapaswa kukuza maisha ya kiroho miongoni mwetu wenyewe (*Msisitizo: waumini wa ujumbe wa malaika wa tatu*). Ulimwengu kwa hekima yake haumjui Mungu. Ulimwengu hauwezi kuona uzuri, urembo, wema, utakatifu wa ile Kweli ya Mwenyezi Mungu. Na ili watu waweze kuielewa hii Kweli, lazima kuwe na mkondo ambao itapitia ili kuja ulimwenguni.Kanisa limekuwa ndio huo mkondo. Kristo hujifunua kwetu, ili tupate kumfunua kwa wengine. Kupitia watu Wake, utajiri wote na utukufu wa karama Yake ile isiyoweza kuneneka hauna budi kufunuliwa. PH130 2.2

Mungu amekabidhi mikononi mwetu kazi takatifu kupita zote, na twahitaji kukutana pamoja ili kupokea mafundisho, ili tuweze kufaa kufanya kazi hii. Twahitaji kuelewa ni sehemu gani ambayo sisi mmoja mmoja tutaitwa kwenda kutenda katika kuijenga

kazi ya Mungu duniani, katika kutetea sheria takatifu ya Mungu, na kumwinua Mwokozi kama "Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Twahitaji kukutana pamoja na kupokea mguso wa Bwana, ili tuweze kuelewa kazi yetu majumbani. Wazazi wanapaswa kuelewa jinsi wanavyoweza kuwatuma wana na binti zao toka katika patakatifu pa nyumbani, wakiwa wamefunzwa, na kuelimishwa haswa, ili waje kufaa kung'aa ulimwenguni. Tunahitaji kuelewa kuhusiana na mgawanyo wa kazi, na jinsi kila sehemu ya kazi inavyopaswa kudumishwa. Kila mmoja anapaswa kuelewa sehemu anayopaswa kutenda, ili kuwe na upatanifu katika mipango-kazi na katika utendaji unaounganisha wote. PH130 2.3

## Kufikia Watu Wengi.

Katika hubiri la mlimani, Kristo aliwaambia wanafunzi Wake, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango;

nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.” Mathayo 5:14-16.

Iwapo mikutano yetu ya kambi itaendeshwa jinsi inavyopaswa kuwa, kwa hakika itakuwa nuru ulimwenguni. Inapaswa ifanyike katika miji na majiji makubwa ambako ujumbe wa ile Kweli haujatangazwa bado, na inawapasa kuendelea kwa majuma mawili au matatu. Wakati mwingine inaweza kufaa kufanya mkutano wa kambi kwa misimu kadhaa mfululizo mahali pale pale; lakini, kama ilivyo kawaida, mahali pa mkutano panapaswa kubadilishwa mwaka hadi mwaka. Badala ya kuwa na mikutano mikubwa ya kambi katika maeneo machache, vyema zaidi ingeweza kufanyika kwa kuwa na mikutano midogo katika maeneo mengi. Ndivyo kazi itakuwa ikienea daima katika maeneo mapya. Mara tu pale kiwango cha Ukweli kinapoinuliwa katika eneo moja; na kuonekana ni salama

kuwaacha waongofu kwenye imani, sharti tujipange kuingia katika maeneo mengine mapya. Mikutano yetu ya kambi ina nguvu, na inapofanyika mahali ambapo jumuiya inaweza kuamshwa, itakuwa na nguvu kubwa zaidi kuliko pale ambapo, kwa ajili ya kuwafaa watu wetu, inawekwa mahali ambapo, kwa sababu ya mikutano ya nyuma na kukataliwa kwa ile Kweli, mvuto wa wengi umefifishwa. PH130 3.1

Kosa limefanywa katika kufanya mikutano ya kambi katika maeneo ya nje ya mji ambako watu hawapo, na kuendelea mahali pale pale mwaka baada ya mwaka. Hili limefanywa ili kuokoa gharama na watendakazi; lakini uokoaji unapaswa kufanywa katika masuala mengine. Hasa hasa katika maeneo mapya, uhaba wa nyenzo mara nyingi hufanya iwe vigumu kukidhi gharama ya mkutano wa makambi. Uchumi makini unapaswa kutekelezwa hapa, na mipango ya gharama nafuu kubuniwa; kwani mengi yanaweza kuokolewa kwa njia hii. Lakini hebu kazi isidhoofike. Njia hii ya kuwasilisha Ukweli

kwa watu, ni ubunifu wa Mungu wetu Mwenyewe. Wakati roho zinapaswa kushughulikiwa, na Ukweli kuletwa mbele ya wale wasioujua, kazi hiyo haipaswi kuzuiwa kwa sababu ya kuokoa gharama. PH130 4.1

Mikutano yetu ya makambi inapaswa kuendeshwa ili kutimiza kiasi kikubwa zaidi cha wema. Ukweli na uwasilishwe ipasavyo na kuwakilishwa vyema na wale wanaouamini. Ni nuru, nuru ile ya mbinguni, ambayo ulimwengu waihitaji, na chochote kinachodhihirisha Bwana Yesu Kristo ni nuru. PH130 4.2

## Kielelezo

Kila mkutano wa kambi unapaswa kuwa somo lenye umalidadi, mpangilio, na linalovutia. Lazima tuzingatie kwa uangalifu uwekevu, na lazima tuepuke kujionyesha; bali kila kitu kilichounganishwa na eneo la kambi, kinapaswa kuwa nadhifu na chenye mpangilio. Ladha na busara huchangia mengi katika kuvutia watu. Na katika kazi

zetu zote tunapaswa kuwasilisha nidhamu ya mpangilio na utaratibu. PH130 4.3

Kila kitu kinapaswa kupangwa ili kuvutia watu wetu wenyewe na ulimwengu wote kwa utakatifu na umuhimu wa kazi ya Mungu. Kanuni zilizokuwa zikifuatwa katika kambi za Waisraeli ni kielelezo kwetu. Kristo Ndiye alitoa maagizo hayo mahsusi kwa Israeli, Naye aliyakusudia kwa ajili yetu sisi, ambao miisho ya dunia imetufikia. Tunapaswa kujifunza kwa makini maelezo bayana ya Neno la Mungu, na kutekeleza maagizo haya kwamba ni mapenzi ya Mungu. Kila kitu kinachohusiana na kambi na kiwe kimetakaswa, kamilifu na chenye kisafi. Uangalifu mahsusi unapaswa kutolewa kwa mipangilio yote ya usafi, na watu wenye uamuzi makini na utambuzi wanapaswa kuona kwamba hakuna chochote kinachoruhusiwa kupanda mbegu za ugonjwa na kifo kwenye kambi lote. PH130 5.1

Mahema yanapaswa kushikiliwa na nguzo kwa usalama, na wakati wowote kukiwa na dalili ya mvua, kila hema linapaswa kuwa

na mtaro wa kupitisha maji ili yasituame. Kwa hali yoyote ile, hebu mambo haya yasipuuzwe. Ugonjwa mbaya na hata unaoleta kifo huja kwa upuuziaji wa tahadhari hii. PH130 5.2

Tunapaswa kuhisi kwamba sisi ni wawakilishi wa ile kweli yenye asili ya mbinguni. Tunapaswa kuzionyesha sifa Zake Yeye aliyetuita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Daima tunapaswa kukumbuka kwamba malaika wa Mungu wanatembea kambini, wakitazama utaratibu na mpangilio katika kila hema. Ile idadi yote kubwa ya watu wanaokuja kwa kufuata mipango yote ya kambi, ni kielelezo cha imani na kanuni za wale watu wanaoongoza mkutano. Mikutano hii inapaswa kuwa kielelezo bora zaidi kwa kadri iwezekanavyo. Mazingira yote yanapaswa kuwa somo. Hasa zile hema za familia katika unadhifu na utaratibu wao, zinapaswa kutoa mandhari ya maisha ya nyumbani, ambayo yatakuwa ni mahubiri ya daima kuhusu tabia, desturi na mtindo vya Waadventista wa Sabato. PH130 5.3

# Jinsi ya Kuhakiki Mahudhurio.

Kabla ya mmoja wa mikutano yetu ya kambi, nilionekana usiku mmoja kuwa katika kusanyiko lililokutana kwa ajili ya kushauriana kuhusu kazi iliyopaswa kufanywa kabla ya mkutano wa kambi. Hapa ilipendekezwa kufanyike juhudi kubwa kabla ya mkutano, na kuwekeza gharama kubwa kwa kusambaza matangazo na makaratasi. Mipango ilikuwa ikifanywa kukamilisha hilo, pale Mmoja ambaye ni Mwenye hekima katika shauri aliposema, “Tengenezeni hema zenu, anzeni mikutano yenu, kisha tangazeni, na mengi zaidi yatatimizwa. PH130 6.1

Ukweli kama ulivyonenwa na mhubiri aliye hai utakuwa na mvuto mkubwa kuliko jambo lile lile litakapochapishwa kwenye magazeti. Lakini njia zote mbili zikijumuishwa pamoja, zitakuwa na nguvu kubwa zaidi. Sio mpango bora kuwa na mbinu ile ile tu ya juhudi mwaka baada ya mwaka. Badili mpangilio wa mambo.

Unapotoa muda na nafasi, Shetani yuko tayari kukusanya majeshi yake, na atafanya kazi kuharibu kila roho inayowezekana. Fanya kazi baada ya mkutano wa makambi kuliko hapo awali (*Msisitizo: kabla ya kuanza makambi*). Usiamshe upinzani kabla watu hawajapata fursa ya kusikia Ukweli na kujua wanapinga nini. Ikiwa matbaa inaweza kupatikana ili ifanyiwe kazi wakati wa mkutano, uchapishaji wa vipeperushi, matangazo, na usambazaji wa machapisho, vitakuwa na ushawishi mkubwa! PH130 6.2

Katika baadhi ya mikutano yetu ya makambi, makundi imara ya watendakazi yamepangwa kwenda mjini na katika viunga vyake ili kutawanya machapisho na kuwaalika watu kwenye mikutano. Kwa njia hii mamia ya watu walipatikana kama wahudumu wa kila mara katika nusu ya mwisho ya mkutano wale ambao vinginevyo wasingeichukulia kwa uzito wake mikutano hii. PH130 6.3

Ni sharti tuchukue kila njia inayokubalika ya kuleta nuru mbele ya watu. Vyombo vya

habari na vitumike, na kila namna ya utangazaji itumiwe ili kuvuta usikivu kwenye kazi hiyo. Hili lisichukuliwe kuwa jambo lisilo la lazima. Katika kila kona unaweza kuona mabango na matangazo yanayotoa tahadhari kwa mambo mbalimbali yanayoendelea, baadhi ya matangazo haya yakiwa yenye sifa ya kupingwa zaidi; na wale walio na Nuru ya Uzima wanaridhika na juhudi hafifu za kuita watu wengi kwenye kusikiliza Ukweli. PH130 7.1

Wale wanaovutiwa wanapaswa kukutana na upotoshaji na udangayifu kutoka kwa wachungaji maarufu, nao hawajui jinsi ya kujibu mambo haya. Kweli inayowasilishwa na mhubiri aliye hai inapaswa kuchapishwa kwa njia ya maelezo mafupi ila yenye kina na ya kutosheleza kwa kadiri inavyowezekana, na kusambazwa kote. Kadiri inavyoweza kufanyika, hotuba muhimu zinazotolewa kwenye mikutano yetu ya makambi na zichapishwe katika magazeti. Ndipo Ukweli ambao uliwekwa mbele ya watu wachache unaweza kufikia

wengi zaidi. Hapo ndipo Nuru ya thamani itaangaziwa katika njia ya wale walio gizani. PH130 7.2

Weka nuru yako juu ya kinara, ili iwaangazie wote waliomo nyumbani. Ikiwa kweli imetolewa kwetu, tunapaswa kuifanya iwe wazi kwa wengine ili kwamba waaminifu wa moyo wapate kuitambua na kushangilia katika miale yake angavu. PH130 7.3

Nathanaeli aliomba apate kujua ikiwa ama sivyo yule aliyetangazwa na Yohana Mbatizaji Ndiye Masihi, kama alikuwa kweli Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Alipokuwa akiweka fadhaa zake mbele za Mungu, akiomba kuangaziwa, Filipo alimwita, kwa dhati, na sauti ya shangwe akisema. "Tumemwona Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti." PH130 7.4

Lakini Nathanaeli alikuwa akimnyanyapaa Mnazareti. Kupitia mvuto wa mafundisho ya uwongo, kutokuamini

kuliinuka moyoni mwake, naye akauliza, “Laweza neno jema kutoka Nazareti?” Filipo hakujaribu kupambana na unyanyapaa na kutoamini kwake. Akasema, “Njoo uone.” Filipo alikuwa na hekima; kwa maana, mara tu Nathanaeli alipomwona Yesu, alisadiki kwamba Filipo alikuwa sahihi. Kutokuamini kwake kulifagiliwa mbali, na imani, thabiti, yenye nguvu, na ya kudumu, ikatawala nafsi yake. Naye Yesu aliipongeza imani yenye tumaini ya Nathanaeli. PH130 8.1

Kuna wengi katika nafasi sawa na ile aliyokuwa nayo Nathanaeli. Wana unyanyapaa nao hawaamini kwa sababu hawajakutana kamwe na zile Kweli maalum za siku hizi za mwisho, au na watu wanaozishikilia, na itahitajika kuhudhuria tu kwenye mkutano uliojawa Roho ya Kristo ili kufagilia mbali kutokuamini kwao. Haijalishi ni nini tutakutana nacho, au ni upinzani gani, au ni jitihada gani yapaswa kuwekwa katika kugeuza roho kutoka kwenye Ukweli wa asili ya mbinguni, sisi ni lazima tuitangaze hadharani imani yetu, ili

roho zipate kuona na kusikia, na kusadiki. Kazi yetu ni kusema, kama Filipo, "Njoo uone." Hatupaswi kuweka nuru yetu chini ya pishi, bali juu ya kinara, ili iwaangazie wote waliomo nyumbani. PH130 8.2

Hatuna fundisho lolote ambalo tunataka kulificha. Kwa wale ambao wameelimishwa kushika siku ya kwanza ya juma kama siku takatifu, kipengele kilicho kinyume zaidi na imani yetu ni Sabato ya amri ya nne. Lakini je, Neno la Mungu halisemi kwamba siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako? Na ingawa si jambo rahisi kufanya badiliko linalohitajika kutoka siku ya kwanza hadi ya saba, badiliko hili lazima lifanywe. Nalo lahusisha msalaba; lagongana na maagizo na mazoea ya wanadamu. Watu wenye elimu wamewafundisha watu mpaka wamejaa kutoamini, chuki isiyo na sababu; na tunapaswa kuwaambia watu hawa, "Njoo uone." Mungu anatuhitaji tuutangaze Ukweli, na kuuacha huu Ukweli ugundue makosa. PH130 8.3

## Washiriki wa Makanisa Yetu Wanapaswa Kuhudhuria Mkutano wa Makambi.

Ni muhimu kwamba washiriki wa makanisa yetu wahudhurie mikutano ya makambi. Maadui wa Ukweli ni wengi, na kwa sababu idadi yetu ni ndogo, kadiri iwezekanavyo tunapaswa kuwa kifua mbele katika kuuwasilisha. Mmoja mmoja, unapaswa unufaike na mkutano, na Mungu akuita kuwa wa kwanza katika safu za ile kweli. PH130 9.1

Wengine watasema "Ni gharama kubwa kusafiri, na itakuwa bora kwangu kuokoa pesa, na kuzitoa kwa maendeleo ya kazi ya Mungu pale ambapo panahitajika sana." Usiwaze kwa namna hii; Mungu akuita kuchukua nafasi yako miongoni mwa jeshi la watu Wake. Imarisha mkutano wa makambi kwa kadiri uwezavyo kwa kuhudhuria pamoja na familia yako. Jitahidi sana kuhudhuria mkusanyiko wa watu wa Mungu (*Msisitizo: mikutano ya zoom ni hafifu na si sababu ya kutokwenda makambi*

*labda uwe na sababu ya ugonjwa au shida fulani*). PH130 9.2

Ndugu na dada, ingekuwa bora kwako kuacha biashara yako iteseke kuliko kupuuza fursa ya kusikia ujumbe anaoukusudia Mungu kwa ajili yako. Usitoe kisingizio kitakachoweza kukuzuia kunufika kiroho. Unahitaji kila mwali wa mwanga. Unahitaji kufaa kiasi cha kutoa sababu ya tumaini lililo ndani yako kwa upole na kicho. Usidiriki kukosa fursa kama hiyo. PH130 9.3

Hapo zamani za kale, Bwana aliwaagiza watu Wake kukusanyika mara tatu kwa mwaka kwa ajili ya ibada Yake. Kwenye mikusanyiko hiyo mitakatifu wana wa Israeli walikuja, wakileta nyumbani mwa Mungu, zaka zao, na sadaka zao za dhambi, na sadaka zao za shukrani. Walikutana kusimuliana rehema za Mungu, kutangaza matendo Yake ya ajabu, na kutoa sifa na shukrani kwa Jina Lake. Na walipaswa kuungana katika huduma ya utoaji kafara ambayo ilielekeza kwa Kristo kama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya

ulimwengu. Kwa kufanya hivyo, ndivyo walivyokuwa wakilindwa dhidi ya mamlaka potovu ya ulimwengu na ibada ya sanamu. Imani na upendo na shukrani vilipaswa kuwekwa hai mioyoni mwao, na kwa njia ya ushirika wao pamoja katika huduma hii takatifu, walifungwa karibu zaidi na Mungu na kwa mwingine. PH130 9.4

Katika siku za Kristo, sikukuu hizi zilihudhuriwa na umati mkubwa wa watu toka nchi zote, na laiti zingeadhimishwa vile Mungu alivyokusudia, katika roho ya ibada ya kweli, kupitia wao nuru ya Ukweli ingeweza kutolewa kwa mataifa yote ya ulimwengu. PH130 10.1

Hata wale walioishi mbali na hema la kukutania, zaidi ya mwezi mmoja kila mwaka, ilikuwa lazima wahudhurie makusanyiko haya matakatifu. Bwana aliona kwamba mikusanyiko hii ilikuwa ya lazima kwa maisha ya kiroho ya watu Wake. Walihitaji kuacha mahangaiko yao ya kidunia, na wazungumze na Mungu, na kutafakari mambo halisi, yale yasiyoonekana. PH130 10.2

Ikiwa wana wa Israeli walihitaji kunufaika na makusanyiko haya matakatifu katika wakati wao, ni kwa kiasi gani basi sisi tunayahitaji zaidi katika siku hizi za mwisho za hatari na migogoro? Na ikiwa watu wa ulimwengu wa wakati huo walihitaji nuru ambayo Mungu ameikabidhi kwa kanisa Lake, je, watu wa leo wanahitaji kwa wingi kiasi gani nuru hiyo? PH130 10.3

Huu ndio wakati wa kila mtu kukwea kumsaidia Bwana dhidi ya mwovu (Waamuzi 5:23). Nguvu za adui zinaimarika, na kama watu wa pekee tunatambuliwa isivyo. Tunatamani watu wafahamu mafundisho na kazi yetu. Tunataka wajue sisi ni nani, na nini tunachoamini. Ni lazima tutafute njia ya kuingia kwenye mioyo yao. Jeshi la Bwana na liwepo kwenye eneo la makambi ili kuwakilisha kusudi na kazi ya Mungu. Usiombe kutoa udhuru. Bwana anakuhitaji. Yeye hafanyi kazi Yake bila ushirikiano wa wakala wa kibinadamu. Nenda kwenye mkutano wa makambi, ingawa lazima itakubidi kujitoea mhanga kuamua hivyo.

Nenda na nia ya kufanya kazi. Na ufanye kila jitihada kuwashawishi marafiki zako waende, si kwa niaba yako, bali waende pamoja nawe, kusimama upande wa Bwana na kutii amri Zake. Wasaidie wanaovutiwa kuhudhuria, ikibidi uwape chakula na malazi. Malaika waagizwao kuwahudumia wale walio warithi wa wokovu watafuatana nawe. Mungu atawatendea watu Wake mambo makuu. Atabariki kila juhudi ili kuheshimu kazi Yake na kuiendeleza kazi Yake. PH130 10.4

## Maandalizi Ya Moyo Yahitajika.

Katika mikusanyiko hii lazima tukumbuke daima kwamba nguvu mbili zinatenda kazi. Vita visivyoonekana kwa macho ya wanadamu vinapiganwa. Jeshi la Bwana liko uwanjani pale kambini likitafuta kuongoa roho. Shetani na sinagogi lake pia wanafanya kazi, wakijaribu kwa kila njia kudanganya na kuharibu. Bwana atuagiza, "Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa

maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho" (Waefeso 6:11, 12). Siku baada ya siku vita vinaendelea. Laiti macho yetu yangefunguliwa kuona mawakala wa wema na uovu utendao kazi, kusingekuwapo na kujali mambo madogo-madogo, ubatili, mzaha au utani. Ikiwa wote wangevaa silaha zote za Mungu na kupigana vita vya Bwana kwa nguvu za kishujaa, ushindi ungepatikana ambao ungefanya ufalme wa giza kutetemeka. PH130 11.1

Hapaswi yeyote kwenda kwenye mkutano wa kambi akitegemea kwamba wachungaji au waalimu wa Biblia ndio wanapaswa kufanya mkutano huo kuwa baraka kwao. Mungu hataki watu Wake wategemee wachungaji. Yeye hataki wadhoofishwe kwa kuwategemea wanadamu ili wapate msaada. Hawapaswi kuegemea, kama watoto wasiojiweza, kwa mtu yeyote kama nguzo. Kama msimamizi wa neema ya Mungu, kila mshiriki wa kanisa apaswa

kuhisi wajibu binafsi wa kuwa na uzima na mizizi ndani yake mwenyewe. Wote wanapaswa kuhisi kwamba kwa mafanikio ya mkutano yanawategemea wao wenyewe hasa. Usiseme, sihusiki; kwamba sitakuwa na la kufanya katika mkutano huu. Ujapohisi hivyo, unampa Shetani mwanya wa kutenda kupitia kwako. Ataijaza akili yako kwa mawazo yake, akikupa kitu cha kutenda katika medani zake. Badala ya kukusanyika pamoja na Kristo, utatanga mbali. PH130 12.1

Mafanikio ya mkutano hutegemea uwepo na nguvu za Roho Mtakatifu. Kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho, kila mpenda Ukweli apaswa kufanya maombi. Na kadiri ilivyo katika uwezo wetu, hatuna budi kuondoa kila kizuizi kwa kazi Yake. Roho hawezi kamwe kumiminwa juu yetu wakati tofauti na uchungu kati ya mtu na mwingine vinaendekezwa na washiriki wa kanisa. Wivu, husuda, kushuku maovu, na kunena maovu ni vya Shetani, na kwa hakika vinazuia njia ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kingine katika ulimwengu huu chenye thamani sana kwa

Mungu kama kanisa Lake. Hakuna kitu kama Kanisa Lake Mungu, kinacholindwa Naye kwa uangalifu wa wivu namna hiyo; hakuna jambo linalomchukiza Mungu kama tendo linalodhuru mvuto wa wale wanaomtumikia. Atawahukumu wale wote wanaomsaidia Shetani katika kazi yake ya kukosoa na kukatisha wengine tamaa. PH130 12.2

Wale wasio na huruma, sikitiko, na upendo hawawezi kufanya kazi ya Kristo. Kabla ule unabii—'Wanyonge watakuwa "kama Daudi," na nyumba ya Daudi, "kama malaika wa Bwana,"—haujatimia, watoto wa Mungu sharti waondoe kila wazo la mashaka dhidi ya ndugu zao. Mapigo yao ya moyo lazima yadunde kwa umoja na wenzao. Fadhila za Kikristo na upendo wa kindugu sharti vionyeshwe kwa wingi zaidi. Maneno yanasikika masikioni mwangu, "kusanyikeni pamoja, kusanyikeni pamoja." Ukweli mzito, mtakatifu kwa wakati huu ni kuwaunganisha watu wa Mungu. Tamaa ya ufahari sharti ife. Somo moja la kuigwa lazima limeze mengine yote, nalo ni—je, ni

nani atakaribia kabisa kufanana na Kristo katika tabia, atakayejisitiri kwa Yesu? PH130 12.3

Kristo asema, “Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana.” Kama paliwahi kuwapo mahali ambapo waumini wanapaswa kuzaa sana ni kwenye mikutano yetu ya makambi. Katika mikutano hii, matendo, maneno, roho ya waumini huwekwa alama, na mvuto wao unafikia hata umilele. PH130 13.1

Mabadiliko ya tabia yanapaswa kuwa ushuhuda kwa ulimwengu kuhusu upendo wa Kristo unaokaa ndani yao. Bwana atazamia watu Wake waonyeshe kwamba uweza wa neema ukomboao, waweza kutenda kazi juu ya tabia zenye kasoro, na kuziwezesha zikue katika ulinganifu na kuzaa sana. PH130 13.2

Lakini ili tuweze kutimiza kusudi la Mungu, kuna kazi ya maandalizi inayopaswa kufanywa. Bwana atuagiza tuondoe mioyo yetu ya ubinafsi ambayo ndio mzizi wa mafarakano. Atamani sana kutumiminia

Roho Wake Mtakatifu kwa kiasi kikubwa, na atuagiza tuisafishe njia kwa kujikana nafsi. Ubinafsi unaposalimishwa kwa Mungu, macho yetu yatafunguliwa ili kuona mawe ambayo kwa sababu ya kutofanana kwetu na Kristo yamekuwa kikwazo kwa wengine. Haya yote Mungu atuagiza tuyaondoe. Asema, "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa" Yakobo 5:16. Ndivyo tunavyoweza kuwa na uhakika ambao Daudi alikuwa nao wakati ule alipoungama dhambi yake, akiomba, "Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi. Nitawafundisha wakosaji njia zako, Na wenye dhambi watarejea kwako." Zab. 51:12, 13. PH130 13.3

Pale Neema ya Mungu inapotawala ndani, roho itazungukwa na pumzi ya imani, ujasiri na upendo kama wa Kristo—ambayo ni pumzi inayotia nguvu maisha ya kiroho ya wote wanaoivuta. Ndipo tutakwenda kwenye mkutano wa makambi, si kwa ajili ya kupokea tu, bali hata kutoa.

Kila aliye mshiriki wa pendo la Kristo lenye rehema,—kila aliyeangaziwa nuru na Roho wa Mungu na kuongoka kwenye ile Kweli, atahisi kwamba kwa ajili ya baraka hizi za thamani, awiwa kwa kila mtu anayekutana naye. Wale walio wanyenyekevu moyoni, Bwana atawatumia kufikia roho ambazo wahudumu waliowekewa mkono hawawezi kuzikaribia. Watasukumwa kunena maneno yanayofunua neema ya Kristo iokoayo. PH130 14.1

Na katika kuwabariki wengine, wao wenyewe watabarikiwa. Mungu hutupa nafasi ya kutoa neema kwa wengine, ili atujaze tena neema nyingi. Tumaini na imani vitaimarika kadiri mtendakazi wa Mungu anavyotenda kazi kwa talanta na nyenzo ambavyo Mungu ametoa. Atakuwa na wakala wa mbinguni, kufanya kazi pamoja naye. PH130 14.2

## Biashara Ziahirishwe.

Kwa kadiri inavyowezekana, mikutano yetu ya makambi yapaswa itolewe wakfu kabisa kwa masilahi ya kiroho. Mikutano hii

haipaswi kufanywa kuwa hafla za shughuli za biashara. PH130 14.3

Katika mikutano ya kambi watendakazi walioajiriwa hukusanywa kutoka maeneo yote ya kazi, na inaonekana kuwa fursa nzuri kwa kuzingatia masuala ya biashara yanayohusiana na matawi mbalimbali ya kazi, na kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi katika nyanja tofauti. Maslahi haya anuwai ni ya muhimu, lakini pale yanapokuwa yameshughulikiwa katika mkutano, ni sehemu ndogo tu ya wakati na juhudi ambayo inahusika katika kushughulikia uhusiano wa kivitendo na roho za watu. Wahudumu hugeuzwa kuiacha kazi yao ya kuwajenga watoto wa Mungu katika imani takatifu zaidi, na mkutano wa kambi haufikii hatima iliyowekwa. Mikutano mingi ambayo huendeshwa wakati wa makambi ni ile ambayo watu wana shauku ndogo nayo, na ikiwa wangeweza kuihudhuria yote, basi wangerudi majumbani mwao wakiwa wamechoka badala ya kuburudishwa na kufaidika. Kwa hivyo wengi hukatishwa

tamaa na kushindwa kwa matarajio yao kuupokea msaada kutoka kwa mkutano wa makambi. Wale waliokuja kwa ajili ya kupata nuru na nguvu hurudi nyumbani kwao wakiwa wamefaa kidogo tu katika kufanya kazi kwenye familia zao na makanisani kwao, kuliko walivyokuwa kabla ya kuhudhuria mkutano. PH130 14.4

Masuala ya biashara yanapaswa kushughulikiwa na wale watu mahsusi walioteuliwa kwa ajili ya kazi hii, na, kadiri inavyowezekana, yapaswa kuletwa mbele ya watu kwa wakati mwingine na si kwenye mkutano wa kambi. Maelekezo ya kutawanya machapisho, katika kazi ya shule ya Sabato, na maelezo ya kina ya vijuzuu na kazi ya kimishonari, yanapaswa kutolewa katika makanisa mahalia au katika mikutano maalum iliyopangwa. Kanuni hiyo hiyo inatumika pia kwa shule za mapishi. **Hizi zikiwapo, zisipaswe kutumia muda katika mkutano wa makambi. PH130 15.1**

Wakuu wa majimbo na wachungaji wanapaswa kujitoa kwa ajili ya masilahi ya

kiroho ya watu, na kwa sababu hiyo, wanapaswa kuachiliwa kutoka kwenye majukumu yao ya kila siku, na kuhudhuria kwenye mkutano wa kambi. Wachungaji na wawe tayari kuwa walimu na viongozi katika kazi iliyo kambini pale inapohitajika, lakini wasichoke. Wanapaswa wajisikie kuburudishwa, na kuwa katika hali ya uchangamfu wa akili; kwa maana hili ni muhimu kwa manufaa bora ya mkutano wa makambi. Wanapaswa kuwa na uwezo wa kusema maneno ya uchangamfu na ujasiri, na kuangusha mbegu za Ukweli wa kiroho katika udongo wa mioyo minyofu ili kuchipuke mimea na kuzaa matunda ya thamani. PH130 15.2

Mhudumu anapaswa kuwafundisha watu jinsi ya kuja kwa Bwana, na jinsi ya kuwaongoza wengine Kwake. Mbinu sharti ziigwe, mipango lazima itekelezwe, ambayo itafanya kiwango kuinuliwa, na watu wanapaswa kufundishwa jinsi wanavyoweza kutakaswa kutokana na uovu, na kuweza kuinuliwa ili kuzingatia kanuni safi na takatifu. PH130 16.1

Lazima kuwe na wakati wa kuchunguza mioyo, kukomaza roho. Akili inapojawa na mambo ya biashara, lazima kuwe na upungufu wa nguvu za kiroho. Utauwa binafsi, imani ya Kweli, na utakatifu wa moyo lazima vidhihirishwe hadi watu watambue umuhimu wake. PH130 16.2

Sharti tuwe na nguvu za Mungu katika mikutano yetu ya makambi, la sivyo hatutaweza kumshinda adui wa roho. Kristo anasema, "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." PH130 16.3

Wale wanaokusanyika kwenye mikutano ya kambi lazima wavutiwe na ukweli kwamba lengo la mikutano hiyo ni kufikia uzoefu wa hali ya juu wa Kikristo, kuendelea katika ujuzi wa Mungu, kuimarishwa kwa nguvu za kiroho; na, pasipo kutambua jambo hili, basi mikutano hii itakuwa isiyo na matunda kwetu. PH130 16.4

## Msaada wa Wachungaji.

Katika mikutano ya kambi, au **mikutano ya hema (tent efforts)**, ndani au karibu na miji mikubwa, kunapaswa kuwapo na msaada tele wa kihuduma. Katika mikutano yetu yote ya kambi kikosi cha wahudumu kinapaswa kuwa na nguvu kadiri iwezekanavyo. Si jambo la hekima kuruhusu mtu mmoja au wawili tu wachoshwe mara kwa mara. Kulazimika hivyo kunawachosha kimwili na kiakili, na wao hawawezi kufanya kazi waliyokabidhiwa kuitenda. Ili mkutano wa kambi upate nguvu zinazohitajika, wahudumu wapaswa kupanga mapema kuacha maeneo yao ya kazi kwenye mikono salama,—pamoja na wale ambao, ingawa hawawezi kuhubiri, wanaweza kuendeleza kazi hiyo nyumba kwa nyumba. Kwa msaada wa Mungu wengi wanaweza kutenda kwa kishujaa; na kwa kazi yao wataona faida, ambayo utajiri wake utawashangaza. PH130 16.5

Katika mikutano yetu mikubwa, karama mbalimbali zinahitajika. Vipawa vipya sharti viletwe kazini. Fursa lazima itolewe,

ili Roho Mtakatifu afanye kazi kwenye akili. Ndipo Ukweli utawasilishwa kwa usafi na nguvu. PH130 17.1

Katika kuendesha masilahi muhimu ya mikutano karibu na mji mkubwa, ushirikiano wa watendakazi wote ni muhimu. Wote wanapaswa kuwa katika mazingira ya mikutano, wakiwatazama watu waingiapo na kutoka, wakionyesha uungwana, adabu na fadhili nyingi sana, na kujali roho za wengine. Wanapaswa kuwa tayari kuzungumza na hizo roho kwa wakati ufaao na usiofaa, wakikesha ili kuzileta roho kwa Bwana. Laiti watenda kazi wa Kristo wangeonyesha kukesha nusu tu ya vile Shetani akeshavyo, ambaye saa zote yuko kuwafuatilia wanadamu, akiwa macho kuweka kileo au mtego wa kuwaangamiza. PH130 17.2

Hebu kila siku inayofuata ifanywe kuwa siku muhimu zaidi ya kazi. Siku hiyo, jioni hiyo, inaweza kuwa fursa pekee ambayo roho fulani inaweza kusikia ile kweli. Zingatia hili daima. PH130 17.3

Wahudumu wanapokubali wenyewe kuitwa mbali na kazi zao na kuyatembelea makanisa, sio tu kwamba wanachosha nguvu zao za kimwili, bali wanajinyang’anya wenyewe muda unaohitajika kwa ajili ya kujifunza na kuomba na wakati wa kutulia mbele za Mungu katika kuichunguza mioyo yao. Na hivyo huwa wasiokidhi kufanya kazi hiyo wakati na mahali inapopaswa kufanywa. PH130 17.4

Hakuna kitu kinachohitajika zaidi katika kazi kuliko matokeo yanayoendana na vitendo vya ushirika na Mungu. Tunapaswa kuonyesha katika maisha yetu ya kila siku kwamba tuna amani na pumziko katika Mungu. Amani Yake moyoni itang'aa usoni mwetu. Nayo itaipa sauti nguvu yenye kuongoa. Ushirika na Mungu utainua maadili kwa tabia na kwenye njia nzima ya utendaji. Wanadamu watatufahamu, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, kwamba tumekuwa pamoja na Yesu. Hili litatoa kwa majukumu ya mhudumu nguvu kubwa zaidi ya ile inayotokana na ushawishi

wa mahubiri yake. Kwa nguvu hii mhudumu sharti asikubali isimpungukie. Ushirika na Mungu kwa njia ya maombi na kujifunza Neno Lake haupaswi kupuuzwa, kwa maana hapa ndipo chanzo cha nguvu zake mwanadamu. Hakuna kazi ya kanisa inayoweza kuchukua nafasi hii. PH130 17.5

Tumejiimarisha kidogo sana kwa Mungu na kwa masuala hakika ya milele. Ikiwa watu watatembea na Mungu, atawaficha mwambani (Kutoka 33). Wakiwa wamefichwa hivyo, wanaweza kumwona Mungu, kama vile Musa alivyomwona. Kwa uweza na nuru ambayo Mungu huwapa, wanaweza kufahamu zaidi na kutimiza zaidi ya walivyokuwa wakidhaniwa kwamba wanaweza. PH130 18.1

Uwezo, busara, na hekima zaidi vyahitajika katika kuwasilisha Neno na kulisha kundi la Mungu kuliko wengi wanavyofikiri. Uwasilishaji mkavu, usio na uhai wa ile Kweli unafanya ujumbe mtakatifu uliootolewa na Mungu kwa mwanadamu udharauliwe. PH130 18.2

Wale wafundishao Neno, lazima wao wenyewe waishi katika mawasiliano ya kila saa, utambuzi, na kuishi katika ushirika na Mungu. Kanuni za Ukweli, haki na rehema lazima ziwe ndani yao. Ni lazima wachote kwenye Chemchemi ya hekima yote, maadili na uwezo wa kiakili. Mioyo yao lazima iwe hai kwa mienendo ya kina ya Roho wa Mungu. PH130 18.3

Chanzo cha nguvu zote hakina kikomo, na ikiwa katika hitaji lako kuu utamtafuta Roho Mtakatifu atende kazi katika nafsini mwako, ukijifungia ndani kwa Mungu, basi ni hakika kwamba hutakuja mbele za watu ukiwa mkavu na usiyehuishwa na Roho. Kwa kusali kwingi na kumtazama Yesu, utaacha kujiinua. Ikiwa unaizoesha imani yako kwa uvumilivu, ukimtumaini Mungu kabisa, utaitambua sauti ya Yesu akisema, “Njoo juu zaidi.” **“Come up higher”** PH130 18.4

## Wote Wawe Watendakazi.

“Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na

waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.” Waefeso 4:11-13.

Andiko hili linatoa wigo mpana wa kazi ambayo inaweza kuletwa katika mikutano yetu ya makambi. Vipawa hivi vyote vyapaswa kutumiwa. Kila mtenda kazi mwaminifu atahudumu kwa ajili ya hatima iliyoonyeshwa, yaani, kuwakamilisha watakatifu. PH130 19.2

Wale ambao wako katika mafunzo ya kufanya kusudi la Mungu katika upande wowote, wanapaswa kuboresha kila fursa ya kufanya kazi kwenye mkutano wa makambi. Popote ambapo mikutano ya makambi inafanywa, vijana ambao wamepata elimu ya umishonari wa kitabibu wanapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wao kutenda. Wanapaswa kutiwa moyo sio tu kufanya kazi katika masuala ya tiba, bali

pia kuzungumza juu ya mambo ya Ukweli wa sasa, wakitoa sababu kwa nini sisi ni Waadventista Wasabato. Vijana hawa wakipewa nafasi ya kufanya kazi na watumishi wakongwe, watapata msaada na baraka nyingi. Kila mtu ana kitu cha kufanya. Kila mtu anayeamini ile Kweli atasimama katika sehemu yake na mahali pake, akisema, "Mimi hapa, Bwana, nitume mimi." Kwa kushiriki katika kazi katika mkutano wa makambi, wote wanaweza kujifunza jinsi ya kufanya kazi kwa mafanikio zaidi katika makanisa yao mahalia. PH130 19.3

Msaada bora zaidi ambao mchungaji aweza kutoa kwa kanisa si katika kuhubiri tu, bali kuwapangia watu kazi. Mpe kila mmoja kitu cha kufanya kwa ajili ya wengine. Waonyeshe kwamba kama wapokeaji wa neema ya Mungu, wote wako chini ya wajibu wa kumfanyia kazi Yeye. Na wote wafundishwe jinsi ya kufanya kazi. Hasa wale walio wapya katika imani, hawa wanapaswa kuelimishwa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Ikiwa wataanza

kazi, wale waliokata tamaa watasahau upesi kufa moyo; wanyonge watakuwa na nguvu, wajinga watakuwa na maarifa, na wote watakuwa tayari kuwasilisha ile Kweli kama iliyo ndani ya Yesu. Kisha watampata msaidizi asiyeshindwa katika Yeye ambaye ameahidi kuwaokoa wote wanaomjia. PH130 19.4

## Sala na Ushauri wa Mara kwa Mara.

Wale wanaofanya kazi katika mikutano ya makambi wanapaswa kushiriki mara kwa mara pamoja katika sala na mashauri, ili waweze kufanya kazi yao kwa akili. Yapo mambo mengi yanayohitaji umakini katika mikutano ya kambi; lakini wachungaji/wahudumu wanapaswa kuchukua muda kukutana pamoja kila siku kwa maombi na mashauri. Unapaswa kujua kwamba mambo yote yanajipanga sawasawa katika mstari, kama maneno yalivyonenwa kwangu—"kwamba umesimama bega kwa bega, ukitembea mbele, na si kuondoka." Kazi inapofanywa kwa namna hii, kuna umoja wa mioyo, na

kutakuwa na maelewano ya kiutendaji. Hii itakuwa njia ajabu ya kuleta baraka za Mungu juu ya watu. PH130 20.1

Kabla ya hubiri tunapaswa kuchukua muda wa kumtafuta Mungu sisi wenyewe. Hiyo ilikuwa desturi yetu katika nyakati za awali. Mara nyingi wachungaji/wahudumu walikuwa wakienda na kuomba pamoja, nao hawakutulia mpaka pale Roho wa Mungu alipojibu maombi yao. Ndipo wangeondoka huku nyuso zao zikiwa zimeng'aa; na walipozungumza na mkutano, maneno yao yalikuwa na nguvu. Walifikia mioyo ya watu, kwa kuwa Roho aliyewapa baraka aliitayarisha mioyo ya kupokea ujumbe. Kuna mengi zaidi yanayofanywa na ulimwengu wa mbinguni kuliko tunavyotambua katika kuandaa njia ambayo roho zaweza kuongoka. Hatuna budi kufanya kazi pamoja na wajumbe wa mbinguni. Tunataka mengi zaidi kutoka kwa Mungu; hatupaswi kuhisi kwamba kuzungumza kwetu na mahubiri yetu ndiyo kunafanya kazi. Watu wasipofikiwa na Mungu, hawatafikiwa kamwe. Hatuna budi

kumtegemea Mungu kikamilifu, tukiomba ahadi Yake, “Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho Yangu, asema Bwana wa Majeshi.” PH130 20.2

Pale ambapo wale ambao Mungu amewakabidhi majukumu kama viongozi, wanapokuwa na kicho na kutetemeka mbele Yake kwa sababu ya wajibu wa kazi hiyo, wanapotambua kutostahili kwao wenyewe, na kumtafuta Bwana kwa unyenyekevu, wanapojitakasa kutokana na yote ambayo hayampendezi, wanapoomba pamoja Naye mpaka pale wanapotambua kuwa wamepata msamaha na amani, basi Mungu atajidhihirisha kupitia kwao. Ndipo kazi itasonga mbele kwa nguvu. PH130 21.1

Watenda kazi wenzangu, ikiwa tutakutana na mafanikio, sharti tuwe na Yesu, Yesu wa thamani, akae mioyoni mwetu kikamilifu zaidi. Twahitaji sana mvuto wa mbinguni, Roho Mtakatifu wa Mungu, ili kutoa nguvu na ufanisi kwa kazi yetu. Twahitaji kufungua mioyo yetu kwa Kristo. Twahitaji imani thabiti zaidi na ibada yenye bidii zaidi. Ubinafsi na ufe, na

katika akili na moyo kuthamini upendo upambao wa Mwokozi wetu. Tutakapomtafuta Bwana kwa moyo wote, tutampata, na mioyo yetu yote itang'ara kwa pendo Lake. Ubinafsi utazama katika kuonekana hauna maana, na Yesu atakuwa yote na katika yote kwa nafsi zetu. PH130 21.2

Kristo atuonyesha sisi tulio na kiu maji ya uzima ili tupate kunywa bure; ndipo tutakuwa na Kristo ndani yetu kama kisima cha maji yakibubujikia uzima wa milele. Ndipo maneno yetu yatatiwa maji. Nasi tutakuwa tayari kuwaburudisha wengine kwa maji. PH130 21.3

Ni lazima tumkaribie Mungu. Ni lazima tuwe watenda kazi pamoja Naye, vinginevyo udhaifu na makosa vitaonekana katika kazi zote tutendazo. Kama sisi tungeachiwa kusimamia maslahi ya kazi ya Mungu kwa njia zetu wenyewe, basi tusingekuwa na sababu ya kutarajia mengi; lakini ikiwa ubinafsi utafichwa katika Kristo, kazi yetu yote itafanywa katika

Mungu. Tuwe na imani kwa Mungu katika kila hatua. Tukiwa tunatambua udhaifu wetu wenyewe, hebu tusiwe wale wasio na imani, bali wale wanaoamini. PH130 22.1

Ikiwa tutamkubali Mungu kwa Neno Lake, basi tutaona wokovu Wake. Injili ile tunayoihubiri ili kuokoa roho zinazoangamia sharti iwe injili ileile inayookoa roho zetu wenyewe. Twapaswa kupokea Neno la Mungu. Ni lazima tule Neno, tuliishi Neno, Neno ni mwili na damu ya Mwana wa Mungu (uhai). Ni sharti tule mwili Wake na kuinywa damu Yake,—kupokea kwa imani tabia za kiroho za Kristo. PH130 22.2

Ni lazima tupokee nuru na baraka, ili tuwe na kitu cha kutoa. Ni fursa ya kila mfanyakazi kwanza kuzungumza na Mungu mahali pa siri pa sala, na kisha kuzungumza na watu kama sehemu ya kinywa cha Mungu. Wanaume na wanawake wanaowasiliana na Mungu, walio na Kristo, huufanya ulimwengu huo kuwa mtakatifu, kwa sababu wanashirikiana na malaika watakatifu. Ushahidi kama huo unahitajika kwa wakati huu. Twahitaji nguvu ya Mungu

ilainishayo, nguvu ya kuwa pamoja na Kristo. PH130 22.3

## Haja ya Kanisa.

Wengi huja kwenye mkutano wa kambi mioyo yao ikiwa imejaa manung'uniko na kulalamika. Kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu, wale wanaojiingiza katika manung'uniko haya lazima waongozwe kuona kwamba ni kosa kwa Mungu. Ni lazima waongozwe kujilaumu wenyewe kwa kuwa wameruhusu adui kutawala akili na maamuzi yao. Kulalamika lazima kugeuzwe kwa toba, kutokuwa na hakika na kukata tamaa lazima kugeuzwe kuwa uchunguzi wa dhati, kwamba nitakuwaje mkweli katika imani? PH130 22.4

Mwanadamu anapokuwa mshiriki wa asili ya Uungu, pendo la Yesu litakuwa kanuni ya kudumu katika nafsi, na ubinafsi katika upekee wake hautaonyeshwa. Lakini inasikitisha kuona wale wanaopaswa kuwa vyombo vya heshima, wakijiingiza katika kujifurahisha katika mambo ya mwilini, na kutembea katika njia ambazo dhamiri

inazihukumu. Watu wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, huanguka hadi kiwango cha chini, daima wakiomboleza juu ya madhaifu yao, lakini kamwe hawamshindi na kumjeruhi Shetani chini ya miguu yao. Hatia na hukumu huifunika roho kila mara, na kilio cha watu kama hao kinaweza kuwa, “maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?” Kwa kuendekeza dhambi, kujiheshimu kunaharibiwa; na hilo likiisha, heshima kwa wengine inapungua; tunabaki kufikiri kwamba wengine si wa haki kama sisi wenyewe. PH130 23.1

Katika mikusanyiko yetu ya kila mwaka mambo haya yanapaswa kuwekwa mbele ya watu, nao wanapaswa kuhimizwa kupata ukombozi katika Kristo dhidi ya nguvu za dhambi. Anasema, “Nanyi mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote, nitaonekana kwenu.” Bendera inapaswa kuinuliwa, na mahubiri yawe ya kiroho zaidi, ili watu wapate kuona sababu ya udhaifu wao na huzuni. Wengi hawana furaha kwa sababu wao si watakatifu. Usafi wa moyo, akili isiyo na kasoro vyaweza kubarikiwa na Mungu

pekee. Dhambi inapoendekezwa, hatima yake ni kutokuwa na furaha tu; na dhambi iletayo matokeo yasiyofurahisha zaidi ni kiburi cha moyo, ukosefu wa huruma na upendo kama wa Kristo. PH130 23.2

## Jinsi Ya Kuwasilisha Ukweli.

Kweli mbalimbali hazifai kuwasilishwa kwa usawa katika kutaniko wakati wowote. Hata Yesu aliwaambia wanafunzi Wake waliokuwa pamoja Naye kwa muda wa miaka mitatu, "Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa" (Yohana 16:12). Ni lazima tujitahidi kueleza hii Kweli, watu wanapokuwa tayari kuisikia na kuthamini uthamani wake. Roho wa Mungu anafanya kazi juu ya akili na mioyo ya wanadamu, na tunapaswa kufanya kazi kulingana na hilo. PH130 24.1

Juu ya baadhi ya Kweli, tayari watu wana ujuzi nazo. Kuna wengine ambao wanavutiwa nazo, na ambao wako tayari kujifunza zaidi. PH130 24.2

Waonyesheni umuhimu wa kina wa hizo Kweli, na uhusiano wake na wengine ambao hawaelewi. Kwa hivyo utaamsha shauku ya nuru zaidi. Hii ilikuwa ni namna ya utendaji wa Paulo. Ni ku—"…tumia kwa halali Neno la Kweli" (2 Timotheo 2:15). PH130 24.3

Kweli na iwasilishwe, si kwa hotuba ndefu zilizo ngumu, bali kwa mazungumzo mafupi, ya moja kwa moja. Unapopitia somo mara moja, usifikiri kwamba unaweza kuendelea moja kwa moja hadi kwenye mambo mengine, ya kwamba wasikilizaji watahifadhi yote ambayo yamewasilishwa. Kuna hatari ya kuharakisha kutoka sehemu moja hadi nyingine. Toa masomo mafupi, kwa lugha rahisi na sahili, na rudia hayo mara kwa mara. PH130 24.4

Usiku mmoja, kabla ya mkutano muhimu, katika saa zangu za kulala niliona nakutana na ndugu zangu, nikimsikiliza Mmoja aliyenena kama Mwenye mamlaka. Naye akasema: "Roho nyingi zitahudhuria mkutano huu ambao kwa dhahiri hawakujua Ukweli utakaotolewa. Watasikiliza na kupendezwa, kwa sababu Kristo

anawavuta; dhamiri inawaambia kwamba yale wanayosikia ni Kweli, kwa kuwa yana msingi katika Biblia. Uangalifu makini wahitajika katika kushughulika na roho hizi. PH130 24.5

"Na viacheni vipengele hivyo vya Kweli vishughulikiwe kwao kadiri wawezavyo kufahamu na kutambua vyema. Ingawa ingeonekana kuwa jambo la ajabu na la kushangaza, wengi watatambua kwa furaha kwamba nuru mpya inatolewa juu ya Neno la Mungu; lakini kama Kweli hii ingetolewa kwa upana sana hata wasiweze kuelewa, wengine wangeenda na wasirudi tena. Wengine wangepotosha Ukweli; katika maelezo yao ya kile kilichosemwa, wangepotosha Maandiko hata kuvuruga akili zingine. Sharti tushughulikie hali hii sasa. Onyesha Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. Si lazima kuwe na roho ya ugomvi au mabishano katika kuitetea ile kweli." PH130 25.1

Wale watakaojifunza namna ya mafundisho ya Kristo na kujielimisha kufuata njia Yake, watavutia na kushikilia

idadi kubwa ya watu sasa, kama Kristo alivyoshikilia watu katika siku Zake. Mwokozi ni kielelezo chetu katika mambo yote. Upendo Wake ukaao moyoni utadhihirishwa katika maneno ambayo yatawafaa wasikiaji, na kuzivuta roho Kwake. Ukweli kwa vitendo unaposisitizwa juu ya watu kwa sababu wewe unawapenda kwa dhati, roho zitasadikishwa, kwa sababu Roho Mtakatifu wa Mungu atasadikisha ukweli. Shetani atakuwa kwenye eneo la makambi, ili kwa uvuli wake mwovu amzinge mwanadamu asimwone Mungu, na hivyo kuzuia kila mwale wa nuru itakayomulika rohoni. Ujumbe mkuu unapaswa kutolewa kama ulivyo katika Yesu. PH130 25.2

Jivikeni unyenyekevu, ombeni ili malaika wa Mungu wakae karibu nanyi ili kuvutia akili zenu; kwa maana si ninyi mnaomtendea Roho Mtakatifu, bali Roho Mtakatifu awatendee. Kuna nguvu ya kushinda, yenye kuvuta kuelekea kwenye injili ya Yesu Kristo; ni Roho Mtakatifu afanyaye Ukweli kuwa wa kuvutia. Tendea

ukweli wa vitendo daima mbele ya watu." PH130 25.3

Usiyaanike yale mambo ya imani yetu ambayo hupingana sana dhidi ya mila na desturi za watu kuwa makubwa na yanayoshamiri mpaka Bwana atakapowapa fursa ya kuitambua kwamba sisi ni waamini katika Kristo, kwamba tunaamini katika Uungu Wake, na Uwepo Wake uliokuwako milele. Watu na waweke mawazoni mwao ushuhuda wa Mkombozi wa ulimwengu. “Mimi Yesu nimemtuma malaika Wangu kushuhudia mambo haya katika makanisa.” PH130 26.1

Jambo la kwanza kabisa na la muhimu zaidi ni kulainisha na kuitiisha roho kwa kumhubiri Bwana wetu Yesu Kristo kama Mwokozi asameheye dhambi. Kamwe mahubiri yasihubiriwe, au mafundisho ya Biblia kutolewa katika mkondo wo wote ule, bila kuwaelekeza wasikilizaji kwa “Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Yohana 1:29. Hatuna budi kuwatangazia watu Kristo na pendo Lake, tukiwasilisha mafundisho yetu

yote kuhusiana na dhamira hii muhimu. Kila fundisho la Kweli humfanya Kristo kuwa kitovu, na kila agizo hupokea nguvu kutoka kwa Neno Lake. PH130 26.2

Weka mbele ya watu msalaba wa Kalwari. Onyesha kile kilichosababisha kifo cha Kristo,—yaani uvunjaji wa sheria. Onyesha kwamba Kristo alikufa ili kuwapa wanadamu fursa ya kuwa raia waaminifu wa ufalme Wake. PH130 26.3

Dhambi haitakiwi kufunikwa, au kutendewa kama jambo lenye uzito mdogo. Dhambi inapaswa kuonyeshwa kama hatia dhidi ya Mwana wa Mungu. Uovu mwingi wa dhambi unapaswa kuwekwa mbele ya watu jinsi ulivyo. Kisha waelekeze kwa Mwokozi aliyeinuliwa, ukiwaambia kwamba kutokufa huja tu kwa kumwamini Kristo, kwa kumpokea kama Mwokozi kwa mtu mmoja mmoja. PH130 26.4

Amsha utambuzi wa watu wanaolala ili kuona jinsi walivyotanga mbali na maagizo ya Bwana kwa kuiga sera za kidunia na kupatana na kanuni za kidunia. Hizi

zimewaingiza katika uvunjaji wa sheria ya Mungu. PH130 27.1

Dhamira kuu ya Kristo ilikuwa tabia ya Baba na upendo mwingi wa Mungu. Pale ulimwengu ulipokosa maarifa ya Mungu, Kristo alikuja kutoa baraka hii isiyopimika. Hii ilikuwa zawadi Yake Mwenyewe kwa ulimwengu wetu, na zawadi hii aliikabidhi kwa wanafunzi Wake ili iwasilishwe nao kwa watu. Karama ile ile na kazi hiyo hiyo imekabidhiwa kwa watumishi Wake hivi leo. PH130 27.2

Wengi katika ulimwengu huu huweka mapenzi yao katika mambo ambayo ndani yake yenyewe si mabaya; lakini wanatosheka na vitu hivi, na hawatafuti mema makuu na ya juu zaidi ambayo Kristo anatamani kuwapa. Sasa, hatupaswi kutafuta kwa nguvu kuwanyima kile ambacho wanakithamini. Wafunulie uzuri na thamani ya ukweli. Waongoze kumtazama Kristo katika uzuri Wake, ndipo watageuka kutoka katika kila kitu ambacho kingeondoa mapenzi yao kutoka Kwake Mwokozi. Hii ndiyo kanuni ya Mwokozi

katika kushughulika na wanadamu; ni kanuni ambayo lazima iletwe ndani ya kanisa. PH130 27.3

Kristo alikuja ulimwenguni ili "kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao" (Isaya 61:1). "Jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa Zake" (Malaki 4:2). Ulimwengu umejaa wanaume na wanawake ambao wamebeba mzigo mzito wa huzuni na mateso na dhambi. Mungu awatuma watoto Wake kuwafunulia Yeye ambaye atawaondolea mzigo na kuwapa pumziko. Ni utume wa watumishi wa Kristo kusaidia, kubariki, na kuponya. PH130 27.4

Unapowafundisha watu, wasilisha mambo machache tu muhimu, na wafanye wasikilizaji waweke umakini kwenye mambo haya. Usilete mawazo yasiyo muhimu katika hotuba zako. Mungu hatakufanya ufikiri kwamba unavutiwa na Roho Wake unapochepuka toka kwenye somo lako, na kuleta mada zisizohusika na zisizo na uhusiano halisi na fungu la Biblia

ulilorejelea. Kwa kutangatanga kutoka kwenye mistari iliyonyooka, na kuleta yale ambayo yanaondoa akili kwenye somo, unapoteza mwelekeo wako na kudhoofisha yale yote uliyosema hapo awali. PH130 28.1

Hubiri Ukweli katika urahisi wake. Usiruhusu mahubiri yako yakumbatie kwa kiasi kikubwa pale ambapo pataonyesha udhaifu badala ya hoja thabiti. Jikite kwenye mambo machache muhimu. Tambua kila wakati ambao ni lazima uwe na uwepo wa Roho Mtakatifu; kwa maana Yeye aweza kufanya kazi ambayo wewe mwenyewe huwezi kuifanya. Wape wasikilizaji wako ngano safi, iliyopepetwa kikamilifu. Wapeni mana ile ile itokayo mbinguni, Naye Roho atashuhudia pamoja na roho yako kwamba si wewe unayenena, bali kwamba Roho Mtakatifu anazungumza kupitia wewe. PH130 28.2

Mwalimu wa Neno sharti kwanza azungumze na Mungu, na ndipo aweze kusimama mbele ya watu huku Roho Mtakatifu akitenda kazi akilini mwake.

Ikiwa ashirikiana na Kristo kwa uaminifu, ahadi hii itatimizwa. “Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” PH130 28.3

Uwe mwangalifu usije ukapoteza utambuzi wa uwepo wa Mwangalizi wa mbinguni. Kumbuka kwamba husemi tu mbele ya kusanyiko la watu, bali mbele ya Yule ambaye unapaswa kumtambua. Ongea kana kwamba ulimwengu wote wa mbinguni u mbele yako. PH130 28.4